**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU MOROGORO**

**'WATU WAPASWA KUFAHAMU'**

## A. KANUNI ZA CHUO

### 1.0 HESHIMA NA UTII

1.1. Kila Mwanachuo ajiheshimu kwa kuweka mwili wake na mavazi yake katika hali ya usafi na heshima. Awe na lugha yenye hadhi ya Ualimu na matendo yake yawe yanakuza heshima ya Ualimu.

1.2. Kila Mwanachuo awaheshimu wenzake, wakufunzi, wafanyakazi wote Chuoni na watu wengine anaokutana nao ndani na nje ya Chuo.

1.3. Kila Mwanachuo ni lazima awe na utii kwa viongozi wa serikali ya Wanachuo, wenzake, wafanyakazi na pia viongozi wengine wa serikali ya Tanzania.

1.4. Kila Mwanachuo anapaswa kuwa mtiifu kwa kengele au ishara yoyote itakayomhitaji kufika mahali anapotakiwa.

1.5. Ni marufuku kwa Wanachuo wa kike kwenda kwenye bweni la Wanachuo wa kiume au Mwanachuo wa kiume kwenda kwenye bweni la wanawake.

1.6. Ni marufuku kwa Mwanachuo kutembelea nyumba za wakufunzi na watumishi wengine wa Chuo bila kibali maalum kutoka kwa mkufunzi wa zamu/Mwadili/ Matron wa Wanachuo.

1.7. Kila Mwanachuo sharti awahi wakati wowote anapohitajika mstarini (assembly), bwaloni, ukumbini, darasani, katika kazi za nje na penginepo mradi ameitwa kwa kengele au ishara nyingineyo.

1.8. Kila Mwanachuo anapaswa kuwa na mazoea ya kusalimu, kusimama kwa heshima, pale inapopasa, na kusema au kufanya jambo kwa namna ya kukweza utu na heshima kulingana na hadhi yao.

1.9. Ni kosa kwa Wanachuo kuonesha kwa njia yoyote ile kwamba wanaishi kama mtu na mpenzi wake, kujiingiza katika tabia za uzinzi na uasherati Chuoni.

## 2.0 USAFI NA AFYA

2.1. Ni marufuku kwa Mwanachuo kuwa na nywele zisizopunguzwa (ndefu sana) au zisizotunzwa vizuri, hii ni pamoja na kucha ndefu, na zilizowekwa rangi, ndevu, kunyoa kipara na meno yasiyopigwa mswaki. Wasichana wanaruhusiwa kusuka nywele zao, lakini hairuhusiwi kutumia kemikali kali katika nywele na ngozi, pamoja na kusuka nywele za rangi au kubadilisha rangi nywele

2.2. Ni lazima kwa Mwanachuo ashiriki kikamilifu katika shughuli zote za kuweka mazingira ya ndani na nje ya mabweni, bwalo la chakula, ukumbi wa mikutano, madarasa na sehemu zingine katika hali ya usafi.

2.3. Ni kosa kwa Mwanachuo kuvuta sigara, bangi, madawa ya kulevya na pombe.

2.4. Ni marufuku kwa mgonjwa kulala bwenini bila idhini ya mganga, Mwadili/Matron au mkufunzi wa zamu au mlezi wa bweni.

2.5. Kabla ya kusajiliwa ni lazima Mwanachuo apimwe awe na cheti cha daktari kutoka katika hospitali ya serikali kinachoonesha kwamba afya yake ni nzuri kwa ajili ya mafunzo ya ualimu.

2.6. Ni kosa kwa Wanachuo wa kike kujaribu au kutoa mimba.

2.7. Hairuhusiwi kwa Mwanachuo wa kike kuwa mjamzito akiwa Chuoni. Endapo itathibitika Mwanachuo huyo ni mjamzito na aliyempa ujauzito ni Mwanachuo wote watalazimishwa kuhairisha masomo mpaka Mwanachuo wa kike atakapojifungua.

2.8. Ni uhalifu kwa Mwanachuo kudhoofisha mwili wake kwa sababu ya uzembe au tabia chafu kama uvutaji wa bangi na matumizi ya dawa za kulevya.

## 3.0 MAVAZI

3.1. Mavazi yanayotakiwa kuvaliwa na Wanachuo wakati wote Chuoni ni lazima yawe ya heshima, safi, na yenye kulingana na utamaduni na hadhi ya Ualimu.

**Wanaume:** Suti nyeusi inayoendana na shati la ‘light blue’ viatu vyeusi vya kutumbukiza na tai nyeusi yenye urefu wa kufika katika mkanda wa suruali au kiunoni.

**Wanawake:** Suti nyeusi yenye sketi ya mshono wa **‘umbo la V’** na shati la rangi ya light blue, viatu vyeusi vya kutumbukiza visivyo na visigino virefu na tai nyeusi inayoishia kifuani.

3.2. Wakati wa vipndi darasani ni marufuku kuvaa kofia/kilemba, viatu vya wazi, bangili, jezi/fulana, headphone, simu isiyozimwa, bukta, sketi fupi na nguo za mipasuo zinazozidi magoti na vitu vinavyofanana na hivyo.

3.3. Mwanachuo sharti avae sare wakati wote anapokuwa nje ya Chuo kwa shughuli za Chuo au zake binafsi, isipokuwa wakati wa rikizo.

3.4. Ni marufuku kwa Mwanachuo kuvaa sare ya Chuo ambayo haikubaliki hapa Chuoni mfano, sare iliyochakaa,

iliyochafuka, au yenye rangi tofauti na rangi iliyopendekezwa na Chuo.

3.5. Kazi za nje, michezo, na nyinginezo nje ya masomo, Mwanachuo atavaa mavazi yanayolingana na shughli hizo.

## 4.0 RUHUSA

4.1. Hairuhusiwi kwenda nje ya Chuo bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mkufunzi wa zamu. Aidha ruhusa zote za kulala nje ya Chuo hutolewa na Mkuu wa Chuo kupitia ofisi ya Uadili.

4.2. Ruhusa ya jumla ya Wanachuo hutolewa siku ya Jumamosi kuanzia saa 4:00 kamili asubuhi hadi saa 10:45 alasiri, na kwa siku ya Jumapili pamoja na siku za sikukuu saa 1:00 asubuhi hadi saa 10:45 alasiri.

4.3. Ni lazima kila mwanachuo kuwahi "**roll call**" kila Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu saa 10:45 alasiri.

## 5.0 RATIBA YA MASOMO

5.1. Kila Mwanachuo anapaswa kushiriki kwenye shughuli nyingine zote zilizopo kwenye ratiba kuu ya Chuo kama vile michezo, vyama vya masomo (club), vikundi vya dini vinavyotambulika n.k.

5.2. Kila Mwanachuo anapaswa kufuata na kuheshimu ratiba kwa kuzingatia muda uliopangwa na shughuli zinazopaswa kufanywa na Mwanachuo huyo.

5.3. Ni marufuku kwa Mwanachuo kuacha kuhudhulia vipindi vya masomo au vya kujisomea kwa mchana/usiku.

5.4. Ni lazima kwa kila Mwanachuo kuwahi na kukaa darasani muda wote anaopaswa kufanya hivyo. Aidha, ni marufuku kwa Mwanachuo wa kozi ya aina yoyote kutoroka darasani au kukaa bwenini kabla ya muda wa masomo kumalizika.

5.5. Ni lazima kwa Mwanachuo kuhudhuria na kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote inayotolewa.

5.6. Ni lazima matokeo ya mazoezi, majaribio, na mitihani inayofanywa yawe mazuri ili kumwezesha Mwanachuo kuendelea na mafunzo ya Ualimu.

5.7. Lazima kila Mwanachuo ajiandae vizuri na afanye mazoezi ya kufundishia kwa njia inayoridhisha.

## 6.0 CHAKULA

6.1 Hairuhisiwi kula chakula chochote nje ya bwalo la chakula.

6.2 Ni marufuku kupika bwenini au mahali pengine popote bila idhini maalum kutoka uongozi wa Chuo.

6.3 Ni marufuku kupeleka chakula bwenini

6.4 Ni marufuku kwa Mwanachuo kumkaribisha mtu yeyote kula chakula cha Wanachuo bila kibali maalum kutoka uongozi wa Chuo

## 7.0 UTUNZAJI WA MALI YA UMMA

7.1 Ni jukumu la kila Mwanachuo kuhakikisha kwamba mali, chombo, au kifaa chochote kinatunzwa na kuhifadhiwa mahali panapohusika.

7.2 Chombo au kifaa chochote cha umma kikipotezwa au kuharibiwa na mtu yeyote hakinabudi kulipwa na aliyehusika. Adhabu kali itatolewa kwa uzembe wa kuharibu mali ya umma katika matumizi kama maji, samani n.k.

7.3 Ni marufuku kwa Mwanachuo kuandika maandishi hovyo hovyo katika majengo au vifaa mbalimbali.

5.8. Ni muhimu kufunga milango ya mabweni wakati wa vipindi vya masomo mchana na usiku na wakati Wanachuo hawapo bwenini.

5.9. Ni marufuku kwa Mwanachuo kutumia vifaa vifuatavyo mabwenini:- vibatali, mishumaa, majagi ya umeme/heater za kuchemshia maji, drier za kukaushia nywele, jiko la umeme, mafuta ya taa na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

## 8.0 WAGENI

8.1 Mwanachuo yeyote anapopata mgeni lazima amfahamishe mkufunzi wa zamu, Mwadili/Matron au mlezi wa bweni mara mgeni anapofika na atoe taarifa mara mgeni anapoondoka.

8.2 Ni marufuku kualika/kutembelewa na wageni siku za masomo au muda wa vipindi vya darasani. Wageni wote wanakaribishwa saa za mchana baada ya masomo, siku za mapumziko na sikukuu za kitaifa. Mwisho wa wageni kuwepo Chuoni ni saa 10:30 jioni.

8.3 Magari ya wageni, pikipiki n.k. lazima viwekwe karibu na lango kuu au sehemu watakazo elekezwa na mlinzi.

## 9.0 MIKUTANO NA MAWASILIANO

9.1 Mikutano yote iliyopangwa na Chuo lazima ihudhuliwe na kila Mwanachuo. Aidha taarifa za misiba, ugonjwa zinazomuhusu Mwanachuo ni lazima zipitie ofisi ya uadili.

9.2 Mikutano mingine yoyote Chuoni lazima ijulikane kwa mkufunzi wa zamu na Mwadili wa Wanachuo kabla ya kufanyika. Tafrija, video, disco, mikutano ya dini n.k. vinaingia katika fungu hili. Si ruhusa kuitisha mikutano bila kibali.

9.3 Wasemaji wa mambo ya Wanachuo kwa uongozi wa Chuo ni **Serikali ya Wanachuo**. Barua au taarifa yeyote ihusuyo kama inatakiwa kupelekwa katika vyombo vya habari (redio, TV, magezeti n.k) lazima zipitie serikali ya Wanachuo na hatimaye kupata kibali kutoka uongozi wa Chuo.

9.4 Ni marufuku kwa Mwanachuo kufungulia redio au chombo chochote cha muziki kwa sauti ya juu kiasi cha kuleta usumbufu kwa wenzake.

9.5 Ikumbukwe kuwa msemaji mkuu wa Chuo ni **Mkuu wa Chuo**.

## 10.0 ULINZI NA USALAMA

10.1 Ni marufuku kwa Mwanachuo kuwa na silaha ya aina yoyote inayoweza kuleta madhara kwa mmiliki na wenzake.

10.2 Kila Mwanachuo anawajibika kujilinda, kulinda mali zake, wenzake na mazingira ya Chuo kwa ujumla.

10.3 Ni muhimu kutoa taarifa mara moja kwa uongozi wa Chuo mara tu kunapotokea au kuonesha tukio/dalili zinazohatarisha usalama au amani Chuoni.

10.4 Mwanachuo haruhusiwi kulaza/kutunza chombo chochote cha usafiri bwenini. Aidha Mwanachuo anayemiliki chombo cha usafiri anapaswa kusajili chombo hicho kwenye uongozi wa Chuo.

**11.0 KAZI**

11.1 Lazima kila Mwanachuo awahi katika kazi yoyote aliyopangiwa.

11.2 Yambidi kila Mwanachuo autumie muda aliopangiwa kufanya kazi aliyopewa na asiondoke kabla ya muda huo bila kibali maalum.

11.3 Kila Mwanachuo aheshimu kazi za mikono na afanye kazi za usafi na kuzalisha mali kwa upeo wa uwezo wake.

**12.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANACHUO KUFUKUZWA CHUO**

11.1 Wizi

11.2 Ulevi

11.3 Kulala nje ya Chuo bila ruhusa

11.4 Kutohudhulia vipindi bila sababu ya msingi

11.5 Kupiga/kupigana

11.6 Kugoma au kushawishi kugoma kwa Wanachuo

**13.0 HITIMISHO**

Endapo sheria zingine zitakiukwa kama zilivyoelezwa adhabu zitatolewa kulingana na uzito wa kosa na wakufunzi/ofisi ya uadili, aidha sheria au makosa mengine ambayo yataonekana kuwa ni magumu/mazito adhabu zake zitatolewa/kuamuriwa na kamati ya nidhamu/maadili.

**B. SHERIA ZA NCHI**

i.) Ni lazima kila mwanachuo afuate maagizo na sheria za serikali (nchi) akijua kwamba kuwa Mwanachuo hakumfanyi aruhusiwe kuvunja sheria za nchi.

ii.) Lazima kila Mwanachuo aheshimu sana alama kuu za Taifa ambazo ni bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, na nembo au ngao ya Taifa.

iii.) Ni kosa kubwa kwa mwanachuo kuchanganya maswala ya siasa na masomo. Chuo ni taasisi ya serikali, hivyo Chuo hakifuati itikadi za chama chochote cha siasa. Chuo kinaendeshwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi.

iv.) Pamoja na kufuata kanuni za Chuo na sheria za nchi, kila Mwanachuo anapaswa kuzifahamu na kuzifuata kanuni, tabia na mwenendo mwema wa mwalimu.